# ninakuabudu mungu wangu.

*traditional song;*
*harmony;shotta nkwera*







**2. Mafahamu yangu yadanganya, ya na po kuona na kugusa.**
**Namsadiki yesu, hadanganyi, yesu mungu mwana na ukweli.**

**3. Waficha umungu msalabani, na ubinadamu altareni.**
**Nami naungama zote mbili, kama mwivi yule mwenye toba.**

**4. Thomas aligusa majeraha, nami nasadiki bila shaka.**
**Ewe yesu nipe pendo lako, tumaini kwako na imani.**

**5. Umeteswa nini bwana mwema, kwa kunipa mkate wa uzima.**
**Yesu ,unifishe ndani yako, ili nilionje pendo lako.**

**6. Yesu Pelikane,nitazame, na kwa damu yako nitakase.**
**Tone moja ndilo linatosha, na dunia yote yaokoka**

**7. ndani ya mafumbo yesu yumo, atafumbulia kwangu lini?**
**nikuone , Yesu uso wako, nishiriki nawe heri yako.**

**AMINA.**